Ugawaji wa Walimu Wapya 2014:

Je, Umezingatia Mahitaji?

Utangulizi

Uhaba wa walimu ni moja ya sababu zinazochangia wanafunzi kushindwa kujifunza vizuri na kuelewa mada za masomo mbalimbali kwa muda muafaka hapa nchini. Katika kukabiliana na changamoto hii, serikali imekuwa ikiajiri walimu kila mwaka na katika mwaka wa fedha 2013/2014 serikali imeajiri jumla ya walimu 17,928 na kuwasambaza katika shule mbalimbali za msingi. Kijarida hiki kinachambua mambo mbalimbali kuhusu hali ya walimu na ugawaji wa walimu wapya katika shule za msingi. Lengo ni kuweza kujibu maswali makuu mawili yafuatayo: Je, hali inabadilika? Je, ugawaji wa walimu unazingatia mahitaji ya walimu kimikoa na kishule?

Hali ya Uwiano kitaifa na kimikoa

Baada ya kuajiri walimu wapya 17,928 mwaka 2014 kwa shule za msingi, tatizo la uhaba wa walimu limepungua. Kitaifa hivi sasa uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi kwa shule za msingi za serikali umepungua toka 1:44 ulivyokuwa mwaka 2013 hadi kufikia 1:40 kwa mwaka 2014 (Chati 1). Hii inamaanisha kwamba hivi sasa mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 40. Licha ya kwamba uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi kitaifa umepungua toka 1:44 hadi 1:40, mikoa 12 (asilimia 48) hasa mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria (Mwanza, Shinyanga, Geita,

Chati 1: Uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi



Simiyu, Mara na Kagera) na mikoa ya kanda ya magharibi (Rukwa, Kigoma na Tabora) bado ina uwiano mkubwa zaidi ya 1:40. Hakuna hata mkoa mmoja kutoka kanda hizi ambao umefikia lengo la kitaifa tofauti na mikoa ya kanda ya mashariki (Pwani, Dar es salaam na Morogoro) na kaskazini (Kilimanjaro, Tanga na Arusha) ambayo yote imevuka lengo la kitaifa la uwiano wa 1:40.(Chati 2 na 4).

Chati 2: Kanda ya Kaskazini



Chati 3: Kanda ya Ziwa



Chati 4:Kanda ya Mashariki



Chati 5: Kanda ya Magharibi



Ugawaji wa Walimu Kimikoa

Ukiangalia mikoa iliyokuwa haina uhaba wa walimu na mikoa yenye uhaba mkubwa wa walimu kabla ya ugawaji wa walimu wapya utagundua kuwa, ugawaji huo hauzingatii haja ya kupunguza matatizo ya ukosefu wa walimu hususani katika mikoa yenye uhaba mkubwa wa walimu. Mwaka 2013 mikoa ya Arusha, Katavi, Morogoro, Pwani, Iringa na Kilimanjaro ndiyo ilikuwa na uwiano kwa wastani wa 1:37 ambao ulikuwa tayari umevuka lengo la kitaifa la kuwa na uwiano wa 1:40. Mikoa ya Mara, Geita na Tabora ndiyo ilikuwa na uhaba mkubwa wa walimu ambapo wastani wa uwiano ulikuwa 1:54; yaani mwalimu mmoja alikuwa anafundisha wanafunzi 54. Cha kushangaza, ni kuwa katika ugawaji wa walimu walioajiriwa mwaka 2014 mikoa ambayo tayari imevuka lengo la kitaifa (Arusha 565, Kilimanjaro 572, Katavi 377, Morogoro 807, Pwani 690 na Iringa 722) imepewa tena walimu wapya 3,733! Hii si sahihi na haikupaswa iwe hivyo kwani uwiano wa mikoa hii umezidi kuwa mzuri zaidi hadi kufikia 1:34 ilhali ule wa mikoa ya Mara, Tabora na Geita bado ni 1:49 ambao bado haujafikia lengo la kitaifa la uwiano wa 1:40.

Chati 5: Mara



Kama walimu 3,733 wangepangwa zaidi kwenye mikoa hii ya Geita, Mara na Tabora yenye uhaba mkubwa wa walimu kila mkoa ungepata walimu 1,244. Hii ingeweza kupunguza tatizo la uhaba walimu kwenye mikoa hii hadi kufikia wastani wa 1:43 kama inavyooneshwa na chati 5, 6 na 7)

Chati 6: Tabora



Chati 7: Geita



Mapendekezo

Serikali Igawe Walimu kwa Kuzingatia Mahitaji

Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi bado ina uhaba wa walimu. Upangaji wa walimu kimikoa, kiwilaya, na kishule lazima uzingatie mahitaji ya walimu kwenye eneo fulani ili ajira hizo ziweze kuboresha mazingira ya ufundishaji darasani.

Kurejesha Hadhi ya Mwalimu

Walimu wengi wanaoajiriwa hawaripoti katika vituo vyao vya kazi kwa sababu ya matatizo yanayowakabili kama vile makazi duni, mishahara midogo, manyanyaso na mazingira magumu ya kufundishia. Hivyo kuna haja ya kuweka mkakati kuhakikisha kuwa walimu hawa wanaripoti kazini na hawaachi kazi ya ualimu. Motisha kama vile nyumba nzuri za kukaa walimu hawa na mishahara haina budi iboreshwe na kuwa kipaumbele katika mkakati huo. Pia serikali itoe motisha zaidi kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu.